



FRONTRUNNER EXAMINATION

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI YA 4 - 2021

SHUGHULI ZA KISWAHILI

4

Jina:

Jinsia: Mvulana Msichana

Jina la shule:.....

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3	Swali la 4
Idadi ya alama	10	10	20	10
Alama sahihi				

1. Kusoma

Soma kisa hiki kwa Sauti. (Alama 10)

Katika kijiji cha Meja, Palikuwa na mzee aliyeitwa Kombo. Kombo alijulikana sana kwa wizi wa kuku wa jirani zake. Kwa ujanja wake hakushikwa akiiba kuku hao.

Usiku mmoja jogoo wa pekee wa mzee koroboi hakuwika. Mzee Koroboi alipowafungulia kuku wake asubuhi hakumwona jogoo wake. Bila shaka alimshuku mzee Kombo kwa wizi wa jogoo wake.

Alipiga ripoti kwa chifu mara moja. Mzee kombo aliposikia ameripotiwa kwa chifu, alimwambia mtoto wake, chifu akija amwambie ameenda safari ya mbali. Mzee Kombo akajificha mvunguni mwa kitanda. Chifu alipomwuliza mtoto baba yake atarudi lini, mtoto aliinama chini ya kitanda na kumwuliza baba yake, "Baba, chifu anauliza utarudi lini?"

2. Ufahamu

(Alama 10)

Soma ufahamu kisha ujibu maswali

Watoto ni muhimu katika jamii. Wao watakuwa viongozi wa siku zijazo. Watoto wakisoma vizuri wataweza kuwa; Wabunge, madaktari, walimu, wahandisi na hata wauguzi.

Watoto wapewe mahitaji ya kimsingi kama chakula, mavazi na makao.

Watoto wapewe elimu na lishe bora wawe na afya. Mtoto ahakikishiwe usalama wake kwa kuelimshwa hadi kiwango cha juu.

Maswali

- a. Mtoto ni muhimu sana katika _____
- b. Watoto watakuwa _____ wa siku zijazo
- c. Mtoto akiwa _____ atawezekutibu wagonjwa.
- d. Mahitaji ya kimsingi ni makao _____ na _____
- e. Lishe bora litawapa watoto _____ njema.

3. Andika majibu ya vitendawili na methali hizi.

- a. Askari mlangoni _____
- b. Nyumba yangu haina mlango _____
- c. Mtoto umleavyo ndivyo _____
- d. Bendera hufuata _____
- e. Pole pole ndio _____
(akuavyo, upepo, kufuli, mwendo, yai)

Andika tarakimu zifuatazo kwa maneno

- a. 210 - _____
- b. 150 - _____
- c. 300 - _____
- d. 20 - _____
- e. 110 - _____

Andika sentensi hizi kwa wakati uliopita

- a. Magari yatapangwa barasteni

- b. Chakula kinapikwa na mpishi

- c. Maji yatakekwa mtoni

- d. Mwashi hujenga nyumba

- e. Samaki anatumia mapezi kuogelea

Chagua jibu sahihi kujaza mianya

- a. Duka la kuuza nyama ni _____
(buchia, buchari, kichinjio)
- b. Panya _____ aliuma nguo yangu
(hiyo, hilo, huyo)
- c. Samaki _____ majini
(hutembea, huogelea, hukimbia)
- d. Vijito _____ vina maji mengi
(hivi, hizi, hizo)
- e. Ng'ombe huishi _____
(kiotani, kondeni, zizini)

4. Kuandika

Andika insha kuhusu "Familia yangu"
